HALMASHAURI YA MANISPAA YA DODOMA

TANGAZO LA ZABUNI

ZABUNI NA LGA/020/2014/2015/NCT/NCS/01

ZABUNI ZA WAKALA WA UKUSANYAJI WA MAPATO KATIKA HALMASHAURI YA MANISPAA YA DODOMA

1. Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma inakusudia kuweka mawakala wa kukusanya Mapato ya Halmashauri na Kupangisha vyumba vya kufanyia biashara (Ghala, migahawa na banda la kuku) kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2014 hadi june, 2015

2. Halmashauri ya manispaa ya Dodoma inapenda kuwaalika watu binafsi, Makampuni, Ushirika, Taasisi au vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria, wenye nia na uwezo wa kuingia mikataba ya kukusanya mapato/kupangisha kutuma maombi yao kwa zabuni zifuatazo:-

Lot.Na.	Chanzo	Na. ya Zabuni
1	Ukusanyaji wa ushuru wa soko la Majengo, Chamwino na Chang'ombe, Bonanza, chadulo	ZABUNI NA LGA/020/2014/2015/NCT/NCS/01
2.	Ukusanyaji wa mapato katika vituo vya mabasi (Kituo kikuu na Jamatini)	ZABUNI NA LGA/020/2014/2015/NCT/NCS/01
3.	Upangishaji na uendeshaji wa mgahawa wa soko la majengo	ZABUNI NA LGA/020/2014/2015/NCT/NCS/01
4	Upangishaji wa Banda la Kuku Miyuji	LGA/020/2014/2015/NCT/NCS/01
5.	Ukusanyaji wa ushuru wa mabango	ZABUNI NA LGA/020/2014/2015/NCT/NCS/01

6.	Upangishaji wa ghala la DODIDECO	ZABUNI NA LGA/020/2014/2015/NCT/NCS/01
7.	Uendeshaji wa huduma ya vyoo vya kulipia	ZABUNI NA LGA/020/2014/2015/NCT/NCS/01
8.	Tozo za huduma (Service levy) toka kwa mashirika/makampuni yanayotoa huduma ndani ya Manispaa ya Dodoma	ZABUNI NA LGA/020/2014/2015/NCT/NCS/01
9	Ada za Maegesho ya magari makubwa na madogo yanayoegeshwa nje ya vituo vya mabasi na Masoko	ZABUNI NA LGA/020/2014/2015/NCT/NCS/01
10	Ukusanyaji wa mapato ya ushuru wa minada ya Manispaa.	ZABUNI NA LGA/020/2014/2015/NCT/NCS/01

MASHARITI YA MAOMBI YA ZABUNI

1. Mzabuni anaruhusiwa kuomba zaidi ya "Lot" moja kwa uwezo wake kila "lot" inajijenga. Mzabuni hataruhusiwa kuomba lot zaidi ya moja kama zabuni moja.

2. **Nyaraka za zabuni zinapatikana baada ya kulipa ada ya kila zabuni husika ambayo ni Shs. 100,000/- Ada hiyo haitarejeshwa (Non refundable).**
3. Ombi la zabuni liwe na jina na anuani ya mwombaji, aidha aoneshe mahali ofisi yake ilipo.
4. Mwombaji aoneshe mchanganuo wa maoteo ya mapato anayotarajia kukusanya, matumizi anayotarajia kuyafanya na kiasi atakachoilipa Manispaa kwa kila mwezi.

   ZINGATIO: Fomu ya maombi ya zabuni ijazwe na kusainiwa na kugongwa mhuri na mwenye uhalali wa kisheria (power of attorney) katika zabuni hii.

5. Mwombaji atatakiwa aambatanishe kivuli cha leseni ya biashara iliyo hai, inayohusika na uwakala wa ukusanyaji wa mapato/madeni /uendeshaji wa huduma ya mgahawa , kivuli cha usajili wa kampuni (kama mwombaji ni kampuni), usajili wa VAT/TIN na "power of attorney" pamoja na bank statement ya kuanzia tarehe 01/12/2013 hadi 31/03/2014 pia aambatanishe vielelezo halali vya kuonesha umiliki wa kampuni hiyo (memorandam na articles of association/extract), kwa mtu binafsi aoneshe "affidavit" iliyopitishwa na mtendaji wa kata au mwanasheria.
6. Mwombaji atakusanya mapato Kwa kuzingatia viwango vilivyopo kwenye sheria ndogo za manispaa ya Dodoma.

7. Mwombaji asiwe na deni lolote analodaiwa na Manispaa ya Dodoma, asiwe na kesi kati yake na Manispaa yeyote inayo husiana na ukusanyaji wa mapato, asiwe amewahi kuvunja mkataba na Mamlaka ya Serikali ya Mitaa kwa kushindwa kutekeleza mkataba kwa uzembe wake au kushindwa kuleta dhamana baada ya kujulishwa ushindi wa zabuni.
8. Mwombaji asiwe amefungiwa kufanya kazi na Mamlaka ya udhibiti wa ununuzi wa umma (PPRA) au mamlaka nyingine.
9. Mwombaji wa zabuni lazima aambatanishe kiapo cha dhamana ya zabuni (bid security declaration). Format yake ipo katika kabrasha la zabuni
10. Iwapo mwombaji atashinda zabuni atatakiwa kuwasilisha dhamana ya utendaji kazi (performance bond) yenye thamani sawa na asilimia 25% ya makusanyo ya mwaka mzima katika chanzo husika, kwa njia ya Banker's cheque au Bank Guarantee kutoka bank inayotambulika kisheria au fedha taslimu ndani ya siku 28 baada ya tarehe ya barua ya kujulishwa ushindi wake na endapo mshindi wa zabuni atashindwa sharti hili ushindi wake utafutwa na kupewa mshindi wa pili au zabuni kutangazwa upya.

11. Mwombaji aambatanishe kuvuli cha stakabadhi ya ada ya maombi ya zabuni

12. Mwombaji aoneshe vifaa alivyonavyo, idadi ya wafanyakazi na uzoefu wao (ambatanisha cv zao). Pia mwombaji aoneshe uzoefu alionao katika kazi anayoiomba usio pungua miaka miwili.

13. Mwombaji aandike juu ya bahasha na kwenye barua ya maombi aina na namba ya zabuni anayoiomba pamoja na "lot" aliyoomba. Juu ya bahasha kusiandikwe wala kuwekwa alama yoyote zaidi ya jina la zabuni, namba ya zabuni, namba ya "lot" na anuani ya Mkurugenzi
14. Mwombaji atatakiwa kuthibitisha kisheria kuwa yeye si mtumishi wa Serikali (public officer) na kuwa hana mgongano wa maslahi (Conflict of interest) katika zabuni anayoiomba kwa kuambatanisha "affidavit".
15. Mwombaji yeyote atakayeshindwa masharti ya zabuni atakuwa amejiondoa katika ushindani.

16. Kwa zabuni ya uendeshaji wa vyoo vya kulipia mwombaji awe na ufahamu na uzoefu wa kutosha kuhusu usafi wa vyoo na atoe maelezo ya jinsi atakavyodumishaUsafi wa choo husika.

17. Muda wa kutembelea maeneo kabla ya kujaza zabuni ni kama ifuatavyo:
    a. Masoko na mgahawa 28/04/2014 kuanzia 3:00 asubuhi – mhusika – afisa biashara wa Manispaa.
    b. Maegesho ya magari, mabango – 29/04/2014 kuanzia saa 3:00 asubuhi – mhusika-mhandisi wa Manispaa.
    c. Vyoo vya kulipia - 29/04/2010 – kuanzia 3:00 asubuhi mhusika – mhandisi wa mazingira/Afisa Afya wa Manispaa.

18. Manispaa hailazimiki kuchagua zabuni yeyote na ina uwezo wa kufuta zabuni kabla au baada ya mchakato wa zabuni kukamilika.

19. Zabuni zote zitumwe zikiwa zimefungwa ndani ya bahasha iliyofungwa ipasavyo. Juu ya bahasha ioneshwe aina ya zabuni namba ya zabuni “lot”. Zabuni zitumwe kwa mkurugenzi kwa anuani ifuatayo:-

    Mkurugenzi wa Manispaa, Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma S.L.P

    1249 DODOMA.

Kwa maelezo zaidi fika katika ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Dodoma, Kitengo cha Manunuzi

20. Maombi ya zabuni zote yatumbukizwe ndani ya sanduku la zabuni lililopo katika ofisi ya Kitengo cha manunuzi, iliyopo ndani ya karakana ya Manispaa ya Dodoma. Mwisho wa kupokea maombi hayo ni tarehe 23.05.2014.saa 4:30 asubuhi (saa za Afrika mashariki). Waombaji au wawakilishi wote, wanaalikwa kuhudhuria ufunguzi wa zabuni hizo utakaofanyika tarehe 23.05.2014 saa 4:30 asubuhi katika ofisi ya Kitengo cha Manunuzi - Manispaa ya Dodoma.

MKURUGENZI WA MANISPAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA DODOMA